# Serikali kujenga majosho 178

NA MWANDISHI WETU, *BUNDA*

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imepanga kujenga majosho ya kuogeshea ng'ombe 178, ili kuiepusha mifugo na magonjwa yanayosababishwa na kupe na maradhi mengine yanayoambatana na kutoogesha mifugo hiyo.

Imesema majosho hayo imepanga kuyajenga katika mwaka huu wa fedha 2021/2022.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, Wilayani Bunda, Mkoani Mara, wakati wa ziara yake ya kukagua miundombinu ya majosho.

Akizungumza na wafugaji wanaofanya shughuli zao katika vijiji vya Salamakati na Kisarakwa vilivyoko Wilayani humo, Ndaki alibainisha kuwa lengo la serikali ni kuweka josho katika kila kijiji kilicho na ng'ombe.

"Josho ni Zahanati ya Mifugo, hivyo sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunataka tuweke kila mahali, ili wafugaji waogeshe mifugo yao kuepukana na kupe na magonjwa mengine yanayotokana na kutoogesha mifugo," alisisitiza.

Aliongeza kuwa mipango iliyopo ni kuendelea kuifanya mifugo iwe na afya njema, jambo ambalo litasaidia kuongeza tija katika ufugaji na kuuza mifugo kwa bei nzuri.

Aidha, aliwataka wafugaji na wananchi kwa ujumla kuendelea kutunza miundombinu ya majosho iliyopo katika maeneo yao na ile itakayojengwa kwasababu kufanya hivyo, kutasaidia uogeshaji wa mifugo kuwa endelevu.

Mbunge wa Bunda, Boniphace Getere, alimwomba Waziri Ndaki kuhamishia fedha za ujenzi wa majosho katika Halmashauri, ili iwe rahisi kuzifuatilia tofauti na ilivyo sasa ambapo zinatoka Wizarani, jambo ambalo linaleta ugumu katika ufuatiliaji wake, hivyo kusababisha miradi ya ujenzi wa majosho kuchelewa kumalizika.

Scanned with CamScanner

... Mwanda hicho, Guy Williams na Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Hanji Godi- ... wakati alipotembelea hivi karibuni

# Serikali yakusudia kujenga majosho 178

**Na Mbaraka Kambona,**
BUNDA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepanga kujenga majosho ya kuogeshea ng'ombe 178, ili kuiepusha mifugo na magonjwa yanayosababishwa na kupe na maradhi mengine yanayoambatana na kutokuogesha mifugo hiyo.

Waziri Ndaki aliyasema hayo katika ziara yake ya kukagua miundombinu ya majosho iliyopo katika Wilaya ya Bunda, mkoani Mara, juzi. Akiongea na wafugaji wanaofanya shughuli zao katika vijiji vya Salamakati na Kisarakwa katika wilaya hiyo, alisema kuwa lengo la serikali ni kuweka josho kwenye kila kijiji kilicho na ng'ombe. "Josho ni zahanati ya mifugo, hivyo sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunataka tuweke kila mahali ili wafugaji waweze kuogesha mifugo yao kuepukana na kupe na magonjwa mengine yanayotokana na kutokuogesha mifugo," alisema.

Aliongeza kuwa mipango iliyopo ni kuendelea kuifanya mifugo iwe na afya njema jambo ambalo litasaidia kuongeza tija katika ufugaji ikiwamo kuuza mifugo hiyo kwa bei nzuri.

Aliwataka wafugaji hao na wananchi kwa ujumla kuendelea kutunza miundombinu ya majosho iliyopo katika maeneo yao na ile itakayojengwa kwa sababu kwa kufanya hivyo kutasaidia uogeshaji wa mifugo kuwa endelevu. Naye Mbunge wa Bunda, Boniphace Getere, alimwomba Waziri Ndaki kuhamishia hela za ujenzi wa majosho katika halmashauri ili iwe rahisi kuzifuatilia tofauti na ilivyo sasa hela za ujenzi zinatoka wizarani jambo ambalo linaleta ugumu katika ufuatiliaji na kusababisha miradi ya ujenzi wa majosho kuchelewa kumalizika.

Scanned with CamScanner

# Serikali kujenga majosho kila kijiji

**Mwandishi Wetu,** Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Bunda.** Serikali imepanga kujenga majosho ya kuogeshea ng'ombe 178, ili kuwaepusha na magonjwa yanayosababishwa na kupe na maradhi mengine yanayoambatana na kutoogeshwa.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema hayo juzi katika ziara yake ya kukagua miundombinu ya majosho wilayani Bunda, Mkoa wa Mara alipozungumza na wafugaji katika vijiji vya Salamakati na Kisarakwa.

Alisema nia ya Serikali ni kuweka josho kwenye kila kijiji kilicho na ng'ombe.

"Josho ni zahanati ya mifugo, hivyo sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunataka tuweke kila mahali, ili wafugaji waogeshe mifugo yao kuepukana na kupe na magonjwa mengine yanayotokana na kutoogesha mifugo," alisema.

Alisema mipango iliyopo ni kuendelea kuifanya mifugo iwe na afya njema, jambo litakalosaidia kuongeza tija katika ufugaji ikiwemo kuuza mifugo kwa bei nzuri.

Aidha, Waziri Ndaki aliwataka wafugaji hao na wananchi kwa ujumla kuendelea kutunza majosho yaliyopo maeneo yao na yale yatakayojengwa kwa sababu kwa kufanya hivyo kutasaidia uogeshaji wa mifugo kuwa endelevu.

Mbunge wa Bunda, Boniphace Getere alimuomba Waziri Ndaki kuhamishia fedha za za ujenzi wa majosho katika Halmashauri, ili iwe rahisi kuzifuatilia tofauti na ilivyo sasa ambapo fedha za ujenzi zinatoka wizarani, jambo linaloleta ugumu katika ufuatiliaji wake na hivyo kusababisha miradi ya ujenzi wa majosho kuchelewa kumalizika.

Scanned with CamScanner

# Wafugaji sasa waongezewa faini mifugo kuingia hifadhini

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, ametangaza rami kwa wafugaji watakaothubutu kuingiza mifugo katika Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori ya Ilumu watatozwa faini ya Sh 100,000 kwa kila kichwa cha ng'ombe badala ya Sh 50,000.

Uamuzi huo umetolewa baada ya malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wafugaji wakidai kuwa mifugo yao inapoingia Iluma ambako faini ni Sh 50,000 inatolewa na askari wa TANAPA na kisha huingizwa katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ambako tozo yake ni Sh 100,000 kwa kila kichwa cha ng'ombe.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama pamoja na wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Ulanga, mkoani Morogoro, Dk. Ndumbaro, alisema amefikia uamuzi huo ili kuwapa nafasi wafugaji watakaokamatwa wakiwa wameingiza mifugo yao kati ya hifadhi hizo kuamua kulipa kiasi hicho cha fedha kwa uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere au kwa uongozi wa Iluma kwa vile kote faini ni sawa.

Kwa mujibu wa taarifa, Iluma ni hifadhi ya wanyamapori inayomilikiwa jamii ambayo ni muungano wa vijiji 14 ambavyo vilitoa ardhi kwa ajili ya shughuli ya uhifadhi na pia ni hifadhi ambayo inapakana na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

" Habari ya kwamba ng'ombe waliga waliingizwa katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere itakuwa haipo kwa sasa kwa sababu faini ni sawa na ya Hifadhi ya Iluma," alisisitiza Dk. Ndumbaro.

Alisema kumezuka tabia ya wafugaji kujichagulia kiasi cha faini ya kulipa mifugo yao inapokamatwa ndani ya hifadhi hiyo na kusisitiza kuwa jambo hilo kamwe halikubaliki.

Alisema mfugaji atakayekuwa na hatia hana haki ya kuchagua adhabu, huku akisisitiza kuwa hali hiyo imesababisha wafugaji kusema uongo kuwa ng'ombe wao wanapokamatwa katika Hifadhi ya Iluma waswagwa katika Hifadhi ya Nyerere ambako faini yake ni kubwa, jambo ambalo sio kweli.

"Kwa mamlaka niliyonayo kama Waziri mwenye dhamana, natangaza kuanzia leo faini ni kiasi cha Sh 100,000 kwa kila kichwa cha ng'ombe," alisisitiza Dk. Ndumbaro.

Akitafanua uamuzi huo wa kutoza Sh 100,000 kwa kila kichwa cha ng'ombe atakayekutwa ndani ya Hifadhi ya Iluma, Dk. Ndumbaro alisema anatumia faini hiyo kutoka katika kifungu cha sheria kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) ...

# Ulaji wa samaki kwa wananchi kuongezeka

**Na BARAKA LOSHILAA**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, amesema utekelezaji wa mradi wa FISH4ACP katika Ziwa Tanganyika mkoani Kigoma, utasaidia ongezeko la ulaji wa samaki kutoka kilogramu 8.5 hadi 10.5 kwa kila Mtanzania kwa mwaka

Mradi wa FISH4ACP unalengo la kuboresha mnyororo wa thamani wa dagaa, lumbu na mgebuka Ziwa Tanganyika, kwa mwaka 2022-2024 ambapo utekelezaji wake ni kupitia Shirika la Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na kuratibiwa na Taasisi ya Utafiti wa Samaki Tanzania (TAFIRI) kwa Ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Shirikishi la Ujerumani

Dk. Tamatamah aliyasema hayo mkoani Kigoma mwishoni mwa wiki iliyopita, akiwa katika warsha ya kutengeneza Mpango wa Mradi wa FISH4ACP ambapo alibainisha kuwa, kupitia mradi huo sekta ya uvuvi itakuwa na maendeleo makubwa kutokana na kugusa maisha ya wananchi walio chini.

"Mradi huu utaongeza kiwango cha ulaji wa samaki ambapo kwa takwimu za FAO, kwa sasa mtu mmoja anakula kilogramu 8.5 kwa mwaka, pia kipato cha wananchi kitaongezeka na kuondokana na umasikini," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Emmanuel Bulayi, alisema mradi wa FISH4ACP utachangia mageuzi makubwa ya kiuchumi Ziwa Tanganyika.

Alisema mradi huo una manufaa katika kuongeza thamani ya samaki Ziwa Tanganyika, kutokana na kugusa watu wote walio katika mnyororo wa thamani.

Bulayi alibainisha kuwa, mradi huo unagusa wavuvi, kinamama wachakataji, wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi hadi katika masoko ya kimataifa, hivyo ni vyema wataalamu watumike kutoa elimu ili mradi huo uonyeshe tija.

Alisema ili kuja na mipango ambayo itawanufaisha wananchi waliopo katika mnyororo wa thamani, ni vyema wataalamu watumike kutoa elimu,

"Zipo changamoto ambazo wananchi wanaziieta wizarani na hazina majibu ya kisayansi, mwaka 2020 kwa kutumia matokeo ya utafiti wa Ziwa Tanganyika, tulibadilisha kanuni na kanuni zile hazikueleweka vyema katika ngazi ya wavuvi, hivyo watafiti wana wajibu wa kuwaelewesha wananchi juu ya kanuni zile," alisema.

Bulayi alisema ili mradi wa FISH4ACP kuwa na tija kwa wananchi, wataalamu, wasimamizi katika Halmashauri na sekretarieti ya mkoa wahakikishe wanatumia taaluma zao vyema, kuwasidia wavuvi na wafanyabiashara kuepukana na hasara.

"Muda mwingine hawapati taarifa sahihi ya kufanya uwekezaji, hivyo kujikuta wapo katika maeneo yasiyofaa, hivyo tumekubaliana ushirikishwaji wa wadau ili malengo ya mradi unakuwa endelevu," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya FAO, Mwakilishi Mkazi wa Shirika hilo kwa upande wa Afrika Mashariki, Martin Van Der Knaap, alisema Umoja wa Ulaya uliomba miswada mbalimbali itakayolenga kwa undani kuhusu mnyororo wa thamani wa samaki na mazao mengine ya uvuvi katika maeneo mbalimbali, na kwamba ni miswada 12 tu kati ya zaidi ya 40 ndio ilikubaliwa kuwezeshwa fedha kwa ajili ya utekelezaji, ukiwamo mradi wa FISH4ACP

Scanned with CamScanner